**Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (United Nations Framework Convention on Climate Change - UNFCCC)**

1. **Utangulizi**

Mkataba huu ulianzishwa mwaka 1992 wakati wa kilele cha Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira na Maendeleo uliofanyika Rio De Janeiro, Brazil. Mkataba huu una jumla ya Nchi Wanachama 198. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia mkataba huu mwezi Aprili, 1996. Mkataba ulianza kufanyakazi mwaka 1994.

2. **Itifaki za mkataba**

Mkataba huu una mikataba midogo, ikiwemo Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris ili kuwezesha utekelezaji wa Mkataba.

i. **Itifaki ya Kyoto (The Kyoto Protocol).** Itifaki ya Kyoto ilianzishwa mwaka 1997. Itifaki hii ina jumla ya Nchi Wanachama 192. Itifaki ilianza kufanyakazi mwaka 2005. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Itifaki ya Kyoto mwezi Agosti, 2002.

ii. **Makubaliano ya Paris (The Paris Agreement).** Makubaliano ya Paris yalianzishwa mwaka 2015 mjini Paris, Ufaransa wakati wa mkutano wa 21 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi. Makubaliano haya yana jumla ya Nchi Wanachama 195 na yalianza kufanya kazi mwaka 2016. Tanzania iliridhia Makubaliano ya Paris mwezi Mei, 2018.

3. **Lengo la Mkataba, Itifaki na Makubaliano ya Paris**

- **Lengo la Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi** ni Kuzuia ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ya ikolojia ya Dunia ili kuhakikisha maendeleo endelevu duniani.

- **Lengo la Itifaki ya Kyoto** ni kuzibana kisheria nchi zinazozalisha gesijoto ili kupunguza uzalishaji wake kwa kuwekewa shabaha maalumu ya kiwango cha kupunguza gesijoto kwa asilimia 5 ikilinganishwa na uzalishaji wake wa mwaka 1990.

- **Lengo la Makubaliano ya Paris** ni kushirikisha nchi zote wanachama katika juhudi za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi hasa upunguzaji wa gesijoto kwa angalau chini nyuzi joto 2 au 1.5 na kusaidia nchi zinazoendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuchochea maendeleo endelevu. Utekelezaji unazingatia misingi ya usawa, uwezo na hali ya uchumi wa nchi husika.

## 4. Ushiriki wa mikutano

Majadiliano chini ya Mkataba huu pamoja na mikataba yake midogo miwili hufanyika chini ya Mkutano wa Nchi Wanachama (Conference of the Parties – COP). Mkutano wa kwanza ulifanyanyika mwaka 1995 baada ya kuanza kutumika kwa Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) uliopitishwa mwaka 1992 katika Mkutano wa Dunia wa Mazingira na Maendeleo (Earth Summit) uliofanyika Rio de Janeiro, Brazil.

Tangu wakati huo, mikutano ya COP hufanyika kila mwaka na ndiyo chombo kikuu cha juu cha kufanya maamuzi chini ya UNFCCC, ikisimamia utekelezaji wa Itifaki ya Kyoto (1997) na Makubaliano ya Paris (2015).

Aidha, chini ya UNFCCC zipo Taasisi Tanzu (Subsidiary Bodies – SBs) ambazo zilianzishwa mwaka 1995 ili kusaidia COP kwa masuala ya kiufundi na utekelezaji. Taasisi hizi ni:

i. *Subsidiary Body for Scientific and Technological Advice (SBSTA),* inayoshughulikia masuala ya kisayansi, teknolojia na mbinu za kiufundi; na
ii. *Subsidiary Body for Implementation (SBI),* inayojikita katika masuala ya utekelezaji, ufuatiliaji, ujenzi wa uwezo na masuala ya kifedha.

Mikutano ya SBs hufanyika mara mbili kwa mwaka, mara nyingi sambamba na vikao vya maandalizi ya COP na wakati wa COP yenyewe.

## 5. Majukumu ya nchi wanachama wa mkataba

- **Kuandaa na Kuwasilisha Taarifa za Kitaifa:** Nchi wanachama zinatakiwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za kitaifa kwa Sekretarieti ya UNFCCC zikionesha hali ya uzalishaji wa gesijoto, hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, pamoja na maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa mkataba.

- **Kutekeleza Hatua za Kupunguza Uzalishaji wa Gesijoto:** Nchi zinawajibika kuchukua hatua za kitaifa za kudhibiti na kupunguza uzalishaji wa gesijoto kupitia sera, mikakati na programu mbalimbali ikiwemo matumizi ya nishati safi, ufanisi wa nishati na uhifadhi wa misitu.

- **Kuimarisha Hatua za Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi:** Nchi wanachama zinapaswa kutathmini hatari na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuandaa mikakati ya kukabiliana na athari hizo, hususan kwa jamii na maeneo yaliyo katika mazingira hatarishi, ili kulinda maisha, uchumi na mifumo ya ikolojia.

- **Kuingiza Masuala ya Tabianchi katika Mipango ya Maendeleo:** Nchi zinatakiwa kuzingatia masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika sera, mipango na bajeti za maendeleo ya kitaifa na sekta mbalimbali, ili kuhakikisha maendeleo yanakuwa endelevu na yanayostahimili athari za tabianchi.

- **Kukuza Elimu, Uhamasishaji na Utafiti wa Tabianchi:** Nchi zinahimizwa kuendeleza elimu, uhamasishaji wa umma na utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi ili kuongeza uelewa wa jamii, kujenga uwezo wa kitaifa na kuimarisha maamuzi yanayotokana na ushahidi wa kisayansi.
- **Kushirikiana Kikanda na Kimataifa:** Nchi wanachama zinapaswa kushirikiana na nchi nyingine, mashirika ya kikanda na ya kimataifa katika utekelezaji wa mkataba, ikiwemo kushiriki kikamilifu katika mikutano ya UNFCCC kama Conference of the Parties (COP).

- **Kurahisisha Upatikanaji na Matumizi ya Rasilimali za Kifedha:** Nchi wanachama zinapaswa kuandaa mipango na miradi inayostahiki ili kunufaika na mifuko ya kimataifa ya tabianchi, pamoja na kuhakikisha matumizi bora na yenye uwajibikaji wa rasilimali zinazopatikana.

- **Kuhakikisha Utekelezaji Endelevu na Utoaji wa Taarifa za Maendeleo:** Nchi zinawajibika kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa hatua za tabianchi, ili kuwezesha uwazi, uwajibikaji na uboreshaji wa utekelezaji wa mkataba.

## 6. Faida za mkataba

Uanachama katika Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) pamoja na vyombo vyake, ikiwemo Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris, huleta faida mbalimbali kwa nchi wanachama, zikiwemo:

- Ushiriki katika maamuzi ya kimataifa: Nchi wanachama hupata fursa ya kushiriki kikamilifu katika majadiliano na maamuzi yanayohusu sera, kanuni na miongozo ya kimataifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.
- Upatikanaji wa fedha za tabianchi: Uanachama huziwezesha nchi kupata rasilimali za kifedha kupitia mifuko ya kimataifa kama Green Climate Fund (GCF), Adaptation Fund, na mifuko mingine ya tabianchi kwa ajili ya miradi ya uhimilivu na upunguzaji wa gesi Joto.
- Uhamishaji wa teknolojia: Nchi hunufaika na upatikanaji wa teknolojia rafiki kwa mazingira, ubunifu wa kisayansi na mbinu bora za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.
- Ujenzi wa uwezo wa kitaifa: Kupitia mafunzo, programu za ujenzi wa uwezo na kubadilishana uzoefu, nchi huimarisha taasisi na rasilimali watu katika masuala ya tabianchi.
- Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa: Mkataba hutoa jukwaa la kuimarisha ushirikiano kati ya nchi, mashirika ya kimataifa, sekta binafsi na asasi za kiraia.

- Msaada wa kiufundi na kisera: Nchi hupata mwongozo wa kitaalamu katika kuandaa sera, mikakati na mifumo ya kitaifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.
- Kuhamasisha maendeleo endelevu: Utekelezaji wa Mkataba husaidia nchi kuunganisha ajenda ya tabianchi na vipaumbele vya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mkataba wa UNFCCC unaziwezesha nchi wanachama kukabiliana kwa pamoja na changamoto za mabadiliko ya tabianchi huku zikihakikisha maslahi yao ya kitaifa na maendeleo endelevu yanazingatiwa.